JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

Simu: +255262963470
Barua pepe: ps@mit.go.tz
Barua pepe: gcu@mit.go.tz
Tovuti: www.mit.go.tz
Faksi +255262963117

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa waViwanda,
S.L.P 2996,
40478DODOMA,

TAARIFA KWA UMMA

TATHMINI YA MWENENDO WA UZALISHAJI, USAMBAZAJI NA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI NA BIDHAA NYINGINE MUHIMU NCHINI KWA KIPINDI KINACHOISHIA FEBRUARI 07, 2022

Jumatatu, 07 Februari, 2022, Dodoma.

A. UTANGULIZI :

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kama mnavyofahamu kwa kipindi kirefu pamekuwepo na malalamiko ya Watanzania kuhusu upandaji holela wa bei ya bidhaa mbalimbali hususan vifaa vya ujenzi pamoja na bidhaa nyingine muhimu kama vile mafuta ya kula, sukari, nk. Aidha, kwa kipindi cha mwisho wa mwaka, kulikuwa na uhaba wa vinywaji baridi, hususan soda na juisi. Hali hiyo si tu imeendelea kuongeza gharama za maisha kwa Mtanzania mmoja mmoja, lakini pia imeendelea kuathiri uchumi wa wa Nchi kwa ujumla wake kwa kuongeza gharama za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya kitaifa kama vile madarasa, hospitali pamoja na miradi mingine ya kimkakati.

Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara ni Wizara yenye dhamana ya kusimamia uzalishaji wa viwandani na mwenendo wa biashara za bidhaa mbali mbali. Wizara ililazimika kuchukua hatua za haraka baada ya kuona kuna uhaba wa baadhi ya vifaa vya ujenzi vile vile, bei za vifaa hivyo vilipanda kiholela hususan saruji. Kufuatia hali hiyo Wizara ilichukua hatua za haraka ili kutafuta suluhu ya tatizo hilo.

Hatua hizo ni pamoja na kukutana na wadau muhimu kwenye eneo hili la uzalishaji na usambazaji wa vifaa vya ujenzi ambapo Wizara ilikutana na wazalishaji wakubwa saba wa saruji nchini (wanaozalisha takriban asilimia 82 ya saruji yote inayotumika nchini) tarehe 31 Januari, 2022 katika Ukumbi wa NDC, Dar es Salaam. Tarehe 01 Februari 2022 kilifanyika kikao kati ya Wizara na Wazalishaji wa Nondo Nchini; Aidha, kilifanyika kikao cha pamoja kati ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda, na Biashara na wasambazaji (distributors) wa

bidhaa za ujenzi tarehe 03 Februari, 2022, Dodoma ambapo wawakilishi wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF) na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI) walialikwa na kuhudhuria vikao vyote hivi.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Leo hii nimekutana nanyi, ili kupitia vyombo vyenu vya habari, niweze kutoa mrejesho kwa Umma wa Watanzania kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara zinazolenga kudhibiti upandaji holela wa bei za bidhaa mbalimbali, hususan vifaa vya ujenzi pamoja na kuadimika kwa baadhi ya bidhaa muhimu sokoni.

Taarifa hii ninayoitoa leo itajikita kueleza matokeo ya uchunguzi uliofanywa na Wizara kuhusu mwenendo wa uzalishaji na usambazaji wa vifaa vya ujenzi katika kipindi cha mwezi Novemba 2021 hadi mwezi Februari 2022.

Aidha, mtakumbuka kuwa tarehe 23 Januari 2022, nikiwa Mkoani Shinyanga, nilitoa taarifa kwa umma kuhusu kuadimika kwa vinywaji baridi na hatua zilizochukuliwa na Serikali kudhibiti hali hiyo ambazo napenda kuwataarifu kuwa zimezaa matunda.

B. MWENENDO WA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI

1. Saruji

Ndugu Wanahabari, kwa sasa Nchi yetu ina viwanda kumi na saba (17) vya saruji vyenye uwezo wa kukidhi mahitaji ya saruji hapa nchini. Hata hivyo, matokeo ya uchunguzi yamebainisha kuwa viwanda vya saruji nchini vinazalisha kwa takribani asilimia 58 tu ya uwezo uliosimikwa wa viwanda hivyo. Hii inaashiria kuwa bado viwanda vya ndani vina uwezo wa kuongeza uzalishaji wa saruji ili kukidhi mahitaji ya ndani ya Nchi na kuweka bei shindani ya saruji sokoni.

2. Nondo

Kwa upande wa nondo, Nchi yetu ina viwanda kumi na sita (16) vinavyozalisha nondo vyenye uwezo wa kuzalisha tani 1,082,788 za nondo za ukubwa mbalimbali, kwa maana ya nondo za ukubwa wa*16mm, 12mm, 10mm na 8mm.* Hata hivyo, uchunguzi umeonesha kuwa uzalishaji wa nondo viwandani kwa sasa hauzidi tani 750,000 pekee. Kwa mujibu wa tathmini iliyofanywa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na FCC juu ya uhaba wa vifaa vya ujenzi nchini na upandaji wa bei kiholela ilibainika kuwa ingawa nondo na bidhaa zinazotokana na chuma zinapatikana kwa uchache, bei zake zimeongezeka sana katika kipindi tajwa.

C. MATOKEO YA TATHMINI

Ndugu Waandishi wa Habari, kwa ujumla tathmini iliyofanyika ilibaini masuala ya msingi yafuatayo:

i. Ongezeko holela la bei za vifaa vya ujenzi, hususan saruji na nondo linasababishwa na wazalishaji wa bidhaa husika kufanya uzalishaji banifu na kutokuwa na mfumo wa wazi wa usambazaji wa bidhaa hizo ambapo kuna mnyororo mrefu wa usambazaji wa bidhaa kutoka kiwandani mpaka kumfikia mlaji wa mwisho (***long and bureucratic distribution chain***);

ii. Gharama halisi za uzalishaji wa saruji haiakisiwi katika bei ya saruji iliyopo sokoni ikilinganishwa na uwiano huo katika nchi jirani na kwingineko duniani;

iii. Ongezeko la bei ya saruji na nondo halina uwiano halisi na gharama za usafirishaji na usambazaji;

iv. Bei ya saruji iliyopo sokoni haina uhusiano na mwenendo wa nguvu za utashi wa mlaji na ugavi *(demand and supply forces);* na

v. Kuna ucheleweshwaji wa makusudi wa utoaji wa saruji kutoka viwandani kwenda kwa wasambazaji *(distributors)* na wanunuzi wa ndani, hususan wale wadogo, waliokwishalipia saruji husika tofauti na wanunuzi wa nje ambao hupatiwa saruji kwa urahisi zaidi. Pamoja na mambo mengine, hali hiyo hupelekea wasambazaji hao kupandisha bei za saruji ili kufidia gharama zilizotumika kuchukua mzigo.

D. HATUA ZINAZOCHUKULIWA NA SERIKALI KUDHIBITI ONGEZEKO HOLELA LA BEI ZA BIDHAA

Kwa kuzingatia tathmini hiyo, Serikali inachukua hatua zifuatazo:

i. Ninawaelekeza wazalishaji, wasambazaji na wafanyabishara wa vifaa vya ujenzi kushusha mara moja bei za bidhaa hizo walizopandisha kiholela na kuuza bidhaa hizo kwa kuzingatia gharama halisi za uzalishaji na usambazaji. Agizo hili linahusu pia bei za vinywaji baridi;

ii. Ninazielekeza Mamlaka zote za udhibiti kuchukua hatua kali dhidi ya walimbikizaji na wauzaji kupitia mlango wa nyuma (***black market***) wanaosababisha bei za bidhaa kupanda sokoni, ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinafika sokoni kwa wakati na kwa bei shindani;

iii. Kwa kuwa kitendo cha kupanga bei kati ya washindani ni uhujumu uchumi, ninazielekeza Mamlaka husika kuchukua hatua kali dhidi ya wote watakaobainika kupanga bei kwa bidhaa kwa mujibu wa sheria za Nchi;

iv. Ninawaelekeza wazalishaji kuzalisha bidhaa hizo kulingana na uwezo wa viwanda uliosimikwa ili kukidhi mahitaji ya soko;

v. Ninawaelekeza wazalishaji wa vifaa vya ujenzi kuweka mifumo mizuri ya usambazaji wa vifaa hivyo ili kuzuia kupanda kwa bei kunakoweza kuzuilika; na

vi. Ninawaelekeza Maafisa Biashara wa Mikoa kote nchini waendelee kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa mbalimbali kwenye maeneo yao na kuwasilisha taarifa hizo mara kwa mara Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, kupitia Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, ili itakapobidi hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Napenda kuhitimisha taarifa yangu kwa kuweka wazi; kuwa mwelekeo wa sera za Uchumi wa kuachia nguvu za soko huria katika uendeshaji wa biashara, ikiwa ni pamoja na Serikali kuachana na jukumu la kupanga bei, **hauna maana ya kuondoa jukumu la msingi la Serikali la kusimamia ushindani wa haki kwenye soko.**

Sisi kama Serikali tuna wajibu wa kudhibiti mienendo hadaifu au kandamizi ya wazalishaji wa bidhaa na wafanyabiashara kwenye soko ikiwa ni pamoja na upandishaji holela wa bei.

Hivyo basi, Serikali haitavumilia tabia ya wafanyabiashara wachache kuanzia wazalishaji hadi wasambazaji wenye dhamira ovu ya kuwaumiza wananchi kwa kujiamulia kupandisha bei za bidhaa bila kufuata utaratibu kwa manufaa yao binafsi.

Dkt. **Ashatu Kijaji (Mb.),**
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA